I&M | Bank

hatua bond

Frequently Asked Questions (FAQs)

ENGLISH

SCAN TO INVEST

Approved By:

CMA

Lead Advisor:

iTrust FINANCE

On Your Side

Frequently Asked Questions (FAQs)

This document answers the most common questions about I&M Bank's inaugural Medium-Term Note (MTN) Bond Programme. It is designed to help you understand the opportunity clearly before making any investment decision. For further information, please read the full Information Memorandum (IM).

1. Who is I&M Bank (T) LTD?
I&M Bank Tanzania Limited is a leading commercial bank in Tanzania, providing corporate, retail, and digital banking services. Established in 2010 following the acquisition of CF Union Bank, it is part of the broader I&M Group, a prominent East African financial conglomerate publicly listed on the Nairobi Securities Exchange.

2. What is a bond?
A bond is debt issued by government or corporate entity with a fixed interest payable every year up to maturity.

3. What is the difference between investing in a bond and keeping money in a fixed deposit?
With a bond, you lend money to the issuing institution and receive periodic interest (coupon) payments. Bonds can also be sold on the Dar es Salaam Stock Exchange (DSE) before maturity. In contrast, a fixed deposit keeps your money locked in an account until maturity and usually pays interest only once.

4. What is the I&M HATUA Bond?
This is the first tranche of I&M MTN program intended to raise TZS 20 Billion plus a greenshoe option of TZS 5 Billion. The interest (coupon) for this bond is 13% per annum payable on quarterly basis for 5 years.

5. What benefits do investors get from investing in the I&M HATUA Bond?
- Attractive interest income of 13% per annum
- Interest (coupon) paid quarterly
- No withholding tax on interest income
- Security of invested funds
- Opportunity to sell the bond on the DSE before maturity

6. What is the interest rate of the I&M HATUA Bond?
The interest rate is 13% per annum, paid quarterly.

7. Who can invest in the I&M HATUA Bond?
- Individuals aged 18 and above
- Children (through a parent or guardian)
- Groups and associations
- Corporations and institutions
- Tanzanian citizens and non-citizens
- Joint investors (e.g.spouses)

8. What is the minimum investment amount?
The minimum investment amount is TZS 500,000.There is no maximum limit.

9. What is the tenor of the I&M HATUA Bond?
The bond has a 5-year maturity period.

10. How and when will investors receive their coupon payments and principal?
All payments will be deposited directly into the bank account provided during application, on a quarterly basis.

Frequently Asked Questions (FAQs)

11. Can an investor use someone else's bank account for payments?
No. The account must be in the investor's name.

12. Can the bond be used as collateral for a loan?
Yes. The bond can be used as collateral for a loan with Financial Institutions. Coupon payments can also support loan repayment.

13. How can one apply for the I&M HATUA Bond?
You can apply in two ways:

- **Digitally:** Apply through iTrust's digital platform (Mobile App) or I&M 's web portal. You can also open a CDS account online if you do not already have one.
- **In person:** Complete a physical Application Form at any I&M Bank office or through any Authorized Collecting Agent listed in the Information Memorandum. Provide valid identification documents (National ID, Passport, or NIDA) and bank account details.
- After completing the application, deposit your investment funds into the designated Hatua Bond Collection Account before the offer closes.

14. What is a CDS account?
A CDS (Central Depository System) account electronically records ownership and enables trading of bonds. It is managed by the Dar es Salaam Stock Exchange (DSE).

15. How do I open a CDS account?
If you don't have one, it will be opened using the information you provide in your bond application.

16. Is an I&M bank account required to invest?
No, you can invest using any valid bank account. I&M Bank is recommended for easier coupon and principal payment processing.

17. Can the interest rate change during the bond period?
No. The interest rate is fixed for the entire 5-year period.

18. Can I invest in foreign currency?
No. The bond is denominated in Tanzanian Shillings (TZS). Investors with foreign currency must convert it to TZS first.

19. Can I invest more than once?
Yes. You may invest multiple times during the offer period. All investments will be consolidated under one bondholder name. You may also purchase more bonds later on the secondary market (DSE).

20. What happens in the event of the bondholder's death?
Ownership will be transferred to the legally recognized beneficiary.

21. Will I receive a certificate of ownership?
No physical certificate will be provided. As an investor, you will receive the DSE Holdings statement as proof of your investment.

Frequently Asked Questions (FAQs)

22. Can foreign investors participate?
Yes. Both Tanzanian and foreign investors can buy the I&M HATUA Bond.

23. Can investors choose how often to receive coupon payments?
No. Coupon payments are fixed quarterly. However, other bank products may help with liquidity needs.

24. Can I sell my bond before the maturity date?
Yes. Once listed on the DSE, you may sell some or all of your bonds on the secondary market through a licensed stockbroker at any time before maturity. The price you receive will depend on market conditions at the time of sale and may be above or below your original investment amount.

25. What happens at maturity (on 21st September 2031)?
On the maturity date, your full principal (the original amount you invested) will be repaid directly to your nominated bank account. No further action is required from your side.

26. What if my bank account details change?
You must notify the Registrar (CSD & Registry Company Limited) or your Broker in writing before the relevant Last Day to Register (3 days before each payment date) so that your updated account details can be recorded in time for the next payment.

27. Is the I&M HATUA Bond Shariah-compliant?
No, this issuance (tranche) is not shariah compliant.

For more information:

Email: customer.care@imbank.co.tz
Phone: +255 784 107 999
Website: www.imbank.co.tz

INVESTMENT DISCLAIMER
This FAQ document is provided for general information purposes only and does not constitute an offer to sell, a solicitation, or financial, legal, or tax advice. Prospective investors are strongly encouraged to read the full Information Memorandum (IM) and consult an independent investment advisor, lawyer, or tax professional before making any investment decision. The I&M Hatua Bond carries investment risks, and past performance is not a guarantee of future returns. This Programme has been approved by the Capital Markets and Securities Authority (CMSA) of Tanzania.

I&M | Bank

hatua bond

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

SWAHILI

SCAN TO INVEST

Approved By:

Lead Advisor:

iTrust

On Your Side

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

Hati hii inajibu maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Mpango wa kwanza wa Hatifungani za Muda wa Kati (MTN Programme) wa I&M Bank Tanzania. Imeandaliwa ili kukusaidia kuelewa fursa hii kwa uwazi kabla ya kufanya uamuzi wa kuwekeza. Kwa maelezo zaidi, tafadhali soma Waraka wa Matarajio (Information Memorandum – IM).

1. I&M Bank (T) Ltd ni nani?

I&M Bank Tanzania Limited ni benki ya biashara inayoongoza nchini Tanzania, inayotoa huduma za benki kwa wateja wa biashara, wateja binafsi na huduma za benki kidijitali. Benki ilianzishwa mwaka 2010 kufuatia ununuzi wa CF Union Bank, na ni sehemu ya I&M Group, kundi kubwa la huduma za kifedha Afrika Mashariki lililosajiliwa katika Soko la Hisa la Nairobi (Nairobi Securities Exchange).

2. Hatifungani ni nini?

Hatifungani ni chombo cha uwekezaji kinachotolewa na serikali au taasisi ya kibiashara kwa ajili ya kukopa fedha kutoka kwa wawekezaji. Mwekezaji hulipwa riba yenye kiwango kilichowekwa kwa muda maalum hadi hatifungani itakapofikia ukomo wake (maturity).

3. Kuna tofauti gani kati ya kuwekeza kwenye hatifungani na kuweka fedha kwenye akaunti ya amana ya muda maalum (Fixed Deposit)?

Unapowekeza kwenye hatifungani, unaikopesha taasisi iliyotoa hatifungani na hupokea malipo ya riba (coupon) kwa vipindi vilivyopangwa. Aidha, unaweza kuuza hatifungani yako katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kabla ya kufikia ukomo wake.

Kwa upande mwingine, fedha zinazowekwa kwenye akaunti ya amana ya muda maalum (Fixed Deposit) hubaki zimewekwa kwenye akaunti hadi muda wa amana utakapokamilika, na kwa kawaida riba hulipwa mara moja tu mwishoni mwa kipindi cha amana.

4. Hatifungani ya I&M HATUA ni nini?

Hii ni awamu ya kwanza ya Mpango wa Hatifungani za Muda wa Kati (Medium-Term Note – MTN) wa I&M Bank, inayolenga kukusanya Shilingi bilioni 20, pamoja na chaguo la kuongeza hadi Shilingi bilioni 5 endapo kutakuwa na mahitaji makubwa kutoka kwa wawekezaji.

Hatifungani hii inalipa riba (coupon) ya 13% kwa mwaka, inayolipwa kila baada ya miezi mitatu (kila robo mwaka) kwa kipindi cha miaka 5.

5. Wawekezaji watanufaika vipi kwa kuwekeza kwenye Hatifungani ya I&M HATUA?

Wawekezaji watanufaika kwa:

- Kupata riba shindani ya 13% kwa mwaka.
- Kulipwa riba (coupon) kila robo mwaka.
- Kutolipa kodi ya zuio (Withholding Tax) kwenye mapato ya riba.
- Kuwa na uhakika wa usalama wa fedha walizowekeza.
- Kuwa na fursa ya kuuza hatifungani katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kabla ya kufikia ukomo wake.
- Kupata mapato endelevu kupitia malipo ya riba yanayolipwa kila robo mwaka.

6. Kiwango cha riba cha Hatifungani ya I&M HATUA ni kiasi gani?

Kiwango cha riba ni 13% kwa mwaka, kinacholipwa kila robo mwaka.

7. Kiasi cha chini cha kuwekeza ni kiasi gani?

Kiasi cha chini cha kuwekeza ni TZS 500,000. Hakuna kiwango cha juu cha uwekezaji

8. Hatifungani ya I&M ina muda gani hadi kufikia ukomo wake?

Hatifungani ya I&M HATUA ina muda wa miaka 5 kabla ya kufikia ukomo wake (maturity).

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

9. Wawekezaji watapokeaje riba (coupon) na marejesho ya mtaji, na ni lini?
Malipo yote ya riba (coupon) pamoja na marejesho ya mtaji yatawekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki iliyotolewa wakati wa kufanya maombi ya uwekezaji. Malipo ya riba yatafanyika kila robo mwaka, huku mtaji ukirejeshwa kulingana na masharti ya hatifungani baada ya kufikia ukomo wake.

10. Je, mwekezaji anaweza kutumia akaunti ya benki ya mtu mwingine kupokea malipo?
Hapana. Akaunti ya benki inayotumika kupokea malipo lazima iwe katika jina la mwekezaji mwenyewe.

11. Je, Hatifungani inaweza kutumika kama dhamana ya mkopo?
Ndiyo. Hatifungani inaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za kifedha. Aidha, malipo ya riba (coupon) yanaweza kusaidia katika urejeshaji wa mkopo.

12. Ninawezaje kutuma maombi ya kuwekeza kwenye Hatifungani ya I&M HATUA?
Unaweza kutuma maombi kwa njia mbili:

- Kwa kufika ofisini:

Jaza fomu ya maombi katika tawi lolote la I&M Bank au kupitia Wakala yeyote Aliyeidhinishwa wa Ukusanyaji (Authorized Collecting Agent) aliyebainishwa kwenye Waraka wa Matarajio (Information Memorandum). Utahitajika kuwasilisha kitambulisho halali (Kitambulisho cha Taifa, Pasipoti au NIDA) pamoja na taarifa za akaunti yako ya benki.

- Kidijitali:

Tuma maombi kupitia mfumo wa kidijitali wa iTrust (Mobile App) au kupitia tovuti ya I&M Bank. Ikiwa huna akaunti ya CDS, unaweza pia kuifungua mtandaoni.
Baada ya kukamilisha maombi yako, weka fedha za uwekezaji kwenye Akaunti Maalum ya Ukusanyaji ya Hatifungani ya HATUA kabla ya kipindi cha mauzo ya hatifungani kufungwa.

13. Akaunti ya CDS ni nini?
Akaunti ya CDS (Central Depository System) ni akaunti ya kielektroniki inayotumika kurekodi umiliki wa hatifungani na kuwezesha miamala ya ununuzi na uuzaji wa hatifungani. Akaunti hii inasimamiwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

14. Ninawezaje kufungua akaunti ya CDS?
Ikiwa huna akaunti ya CDS, itafunguliwa kwa kutumia taarifa utakazowasilisha katika fomu yako ya maombi ya kuwekeza kwenye Hatifungani ya I&M HATUA.

16. Je, ni lazima kuwa na akaunti ya I&M Bank ili kuwekeza?
Hapana. Unaweza kuwekeza kwa kutumia akaunti yoyote halali ya benki. Hata hivyo, kutumia akaunti ya I&M Bank kunapendekezwa ili kurahisisha upokeaji wa malipo ya riba (coupon) na marejesho ya mtaji.

17. Je, kiwango cha riba kinaweza kubadilika katika kipindi cha hatifungani?
Hapana. Kiwango cha riba ni cha kudumu kwa kipindi chote cha miaka 5 ya hatifungani.

18. Je, ninaweza kuwekeza kwa fedha za kigeni?
Hapana. Hatifungani hii imetolewa kwa Shilingi za Tanzania (TZS). Wawekezaji wenye fedha za kigeni watapaswa kuzibadilisha kuwa Shilingi za Tanzania kabla ya kuwekeza.

19. Je, ninaweza kuwekeza zaidi ya mara moja?
Ndiyo. Unaweza kuwekeza mara nyingi kadri unavyotaka katika kipindi cha utoaji wa hatifungani. Uwekezaji wako wote utaunganishwa chini ya jina lako moja kama mmiliki wa hatifungani. Pia, unaweza kununua hatifungani zaidi katika soko la upili kupitia DSE baada ya hatifungani kuorodheshwa

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

20. Nini hutokea endapo mmiliki wa hatifungani atafariki?
Umiliki wa hatifungani utahamishiwa kwa mrithi au mnufaika anayetambuliwa kisheria, kwa kuzingatia taratibu na sheria husika.

21. Je, nitapokea cheti cha umiliki?
Hapana. Hutapewa cheti cha umiliki cha karatasi. Badala yake, utapokea taarifa ya umiliki kutoka Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE Holdings Statement) kama uthibitisho wa uwekezaji wako.

22. Je, wawekezaji wa kigeni wanaweza kushiriki?
Ndiyo. Raia wa Tanzania na wawekezaji wa kigeni wanaruhusiwa kuwekeza kwenye Hatifungani ya I&M HATUA.

23. Je, wawekezaji wanaweza kuchagua mara ngapi wapokee malipo ya riba (coupon)?
Hapana. Malipo ya riba (coupon) hulipwa kila robo mwaka kulingana na ratiba iliyowekwa. Hata hivyo, bidhaa nyingine za benki zinaweza kusaidia kukidhi mahitaji ya ukwasi (liquidity).

24. Je, ninaweza kuuza hatifungani yangu kabla ya tarehe ya ukomo (maturity)?
Ndiyo. Baada ya hatifungani kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), unaweza kuuza sehemu au hatifungani zako zote katika soko la upili kupitia dalali wa hisa mwenye leseni wakati wowote kabla ya ukomo wake. Bei utakayopata itategemea hali ya soko wakati wa mauzo, na inaweza kuwa juu au chini ya kiasi chako cha awali cha uwekezaji.

25. Nini hutokea hatifungani inapofikia ukomo wake (tarehe 21 Septemba 2031)?
Katika tarehe ya ukomo, mtaji wako wote (kiasi cha awali ulichowekeza) utarejeshwa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki uliyoteua wakati wa maombi. Hutahitajika kuchukua hatua yoyote zaidi.

26. Itakuwaje ikiwa taarifa za akaunti yangu ya benki zitabadilika?
Lazima umtaarifu kwa maandishi Msajili (CSD & Registry Company Limited) au Dalali wako wa Hisa kabla ya Siku ya Mwisho ya Kusajili (Last Day to Register), ambayo ni siku 3 kabla ya tarehe ya malipo, ili taarifa zako mpya za akaunti zisasishwe kwa wakati kwa ajili ya malipo yanayofuata.

27. Je, Hatifungani ya I&M HATUA inazingatia kanuni za Sharia?
Hapana. Awamu hii ya utoaji wa hatifungani (tranche) haizingatii kanuni za Sharia.

Kwa maelezo zaidi

Barua pepe: customer.care@imbank.co.tz
Simu: +255 784 107 999
Tovuti: www.imbank.co.tz

TAHADHARI KUHUSU UWEKEZAJI
Hati hii ya Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs) imetolewa kwa madhumuni ya kutoa taarifa za jumla pekee. Haipaswi kutafsiriwa kama ofa ya kuuza, mwaliko wa kuwekeza, wala ushauri wa kifedha, kisheria au wa kodi. Wawekezaji watarajiwa wanahimizwa kusoma kwa makini Waraka wa Matajirio (Information Memorandum – IM) na kushauriana na mshauri huru wa uwekezaji, mwanasheria au mtaalamu wa kodi kabla ya kufanya uamuzi wowote wa kuwekeza. Uwekezaji katika Hatifungani ya I&M HATUA unahusisha hatari za uwekezaji, na utendaji wa awali hauhakikishi matokeo au faida za baadaye. Mpango huu umeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Tanzania (Capital Markets and Securities Authority – CMSA).